KABONDO KASIPUL
NG-CDF

BODI YA SERIKALI YA KITAIFA MFUMO WA MAENDELEO MAJIMBONI
# ENEO BUNGE LA KABONDO KASIPUL
**Sanduku La Posta:** 84 - 40223 Kadongo, Kenya, **Simu:** 0721453336
**Barua Pepe:** cdfkabondokasipul@ngcdf.go.ke / cdfkabondokasipul@gmail.com
**Tovuti:** www.ngcdf.go.ke

## HATI YA HUDUMA NA UTENDAKAZI

### MAONO
Eneo bunge ambalo jumuiya zinatumia fursa za maendeleo na kushiriki ufanisi

### MALENGO
Kuendeleza na kuboresha maisha endelevu ya wapiga kura kwa kushirikiana na wadau

### MADILI YA MSINGI
- Kuzingatia Matokeo
- Usawa
- Kushiriki
- Uadilifu

## VIWANGO VYA HUDUMA WAKATI WA KUWASILIANA NA WATEJA WETU

### MAWASILIANO BINAFSI OFISINI

| KANUNI ZA HUDUMA | VIWANGO VYA HUDUMA | MALIPO | MUDA |
|---|---|---|---|
| Tutakuwa na adabu, watendaji wa kazi na wenye kusaidia | • Tutahakikisha kuwa tuna mapokezi ya jumla katika kiingilio chetu ili kuwapokea wateja<br>• Tutakuhudumia kwa muda wa dakika tano (5) pindi tu unapowasili ikiwa ulikuwa umepanga miadi (Ombi la kukutana na kuhudumiwa)<br>• Tutakuhudumia kwa muda wa dakika ishirini(20) pindi unapowasili pasipo miadi<br>• Tutakuarifu mapema ikiwa utachelewa kuhudumiwa | Bila Malipo | Dakika 5 |

### SIMU

| KANUNI ZA HUDUMA | VIWANGO VYA HUDUMA | MALIPO | MUDA |
|---|---|---|---|
| Simu zetu zitajibiwa mara moja. | • Tutahakikisha mawasiliano ya simu zetu ni ya ufanisi<br>• Tutajibu simu yako ikiita | Bila Malipo | Milio tatu |
| Tutakuwa na adabu, watendaji wa kazi na wenye kusaidia | • Tutapojibu simu tutataja majina yetu.<br>• Tutakapo piga simu, tutatoa majina yetu na mahali pa kazi na kusema sababu za kupiga simu. | Bila Malipo | |
| Tutapatikana kupitia simu wakati wa masaa ya kazi. | • Vitengo vyote vya biashara vitakuwa na huduma ya simu wakati wa masaa ya biashara. Kuanzia saa 8 asubui hadi 5 jioni kukiwa na pumziko la chakula cha mchana ya lisaa limoja siku za kazi. Jumatatu hadi Ijumaa. Ofisi zinafungwa Jumamosi, Jumapili, na siku za siku kuu.<br>• Tutajibu jumbe za simu ndani ya siku moja ya kazi. | Bila Malipo | |

### MAWASILIANO YA BARUA NA NYARAKA

| KANUNI ZA HUDUMA | VIWANGO VYA HUDUMA | MALIPO | MUDA |
|---|---|---|---|
| Tutajibu barua au nyaraka zinazohitaji majibu | • Barua au Nyaraka<br>• Tutajibu nyaraka zote kwa kutumia njia mwafaka; simu, baruameme, binafsi au kwa kuandiaka<br>• Unapotutumia ujumbe wa barua meme, tutakutumia ujumbe mfupi kukufahamisha kwamba tumepokea ujumbe wako. Pia tutakujulisha muda ambao tutachukua kukujibu kwa mapana na marefu. | Bila Malipo | Siku 2 baada ya kupokea |

### MAOMBI YA UFADHILI WA KIFEDHA YA MASOMO

| KANUNI ZA HUDUMA | VIWANGO VYA HUDUMA | MALIPO | MUDA |
|---|---|---|---|
| Upokezi wa fomu ya ombi la ufadhili wa fedha ya masomo | • Fomu lililojazwa kuzingatia kanuni iliyorodheshwa kwenye fomu | Bila Malipo | Dakika 5 |
| Ufadhili wa fedha ya masomo | • Fomu za maombi zitapatikana kwenye tovuti na ofisi<br>• Wafadhiliwa watateuliwa kwa kuhusisha umma<br>• Orodha ya waliofaulu kupata ufadhili wa kifedha itawekwa wazi kwenye ubao wa taarifa na sehemu nyinginezo muhimu bila kuchelewa pindi tu pesa zinapotumwa kwa wafadhiliwa<br>• Tutawasilisha fedha kwa waliofaulu kwa haraka na kushughulikia malalamishi yanayoibuka | Bila Malipo | Wiki 2 baada ya kupokea fedha |

### USIMAMIZI WA MIRADI

| KANUNI ZA HUDUMA | VIWANGO VYA HUDUMA | MALIPO | MUDA |
|---|---|---|---|
| Malipo | • Tuta toa malipo ya haraka ikiwa bidhaa na huduma ambazo tumepokea zilizo nzuri zikiwa na nyaraka husika. | Bila Malipo | Ndani ya siku tatu (3) za kazi ya risiti. |
| | • Isipokuwa pale ambapo mkataba wa maandishi ukisema vingine, tutafanya malipo ya bidhaa na huduma zilizotolewa **ndani ya siku thelasini (30) za kalenda** kutoka tarehe ambapo risiti ya Ankara ilitolewa na nyaraka husika zikiwasahihi. | Bila Malipo | Ndani ya siku thelathini (30) za kalenda |
| | • Kukiwa na shaka kuhusu kiasi kinachodaiwa, titamtaarifu muuzaji kuhusu wasiwasi **wetu ndani ya siku saba za kazi** kutoka tarehe ya risiti ya Ankara na kuomba uhakiki. | Bila Malipo | Ndani ya siku saba (7) za kazi |
| | • Tutatatua maoni ya kimaandishi ya wateja tuliyopokea kupitia barua, faksi au ujumbe | Bila Malipo | Ndani ya siku saba (7) za kazi. |
| Maidhinisho ya malipo ya kamati ya usimamizi wa miradi | • Tutakagua stakabadhi zote na kuidhinisha mapokezi ya fedha, ikiwa zinaafikiana na viwango vilivyo orodheshwa na vinavyofaa | Bila Malipo | Ndani ya siku tatu (3) za kazi ya risiti. |
| Zabuni kwa wauzaji wenye uhitimu waawali. | • Tutatumia uhitimu wa awali wa wauzaji na kutumia ushindani wa zabuni katika hatua za manunuzi ya bidhaa na huduma kamailivyo katika sharia ya Manunuzi ya Umma 2015 na taratibu zake.<br>• Tutakuwa wa wazi na watenda haki tutakapokuwa tunashughulika na wauzaji. Tutawahabarisha wenye zabuni wote matokeo ya zabuni. kurekebisha nukuu na kutoa LPO, LSO.<br>• Tutawasiliana ndani ya **siku tatu (3).** Baada ya kumalizika kwa siku 21 muda unaoruhusiwa kwa kutoa zabuni.<br>• Tutachapisha katika tovuti yetu kila robo mwaka mikataba yote iliyotolewa katika muda huo kwa mwaka hadi sasa. | Bila Malipo | Ndani ya siku tatu (3) za kazi ya risiti. |

### MAONI, MAPENDEKEZO NA MALALAMISHI

| KANUNI ZA HUDUMA | VIWANGO VYA HUDUMA | MALIPO | MUDA |
|---|---|---|---|
| Maoni, malalamishi na mapendekezo | • Tutatambua maoni ya wateji wetu<br>• Tutatatua maoni ya wateja tuliyopokea | Bila Malipo | Ndani ya siku tatu (3) za kazi ya risiti. |
| | • Tutatatua maoni ya wateja tuliyopokea kupitia tovuti, barua pepe, maandishi na simu | Bila Malipo | Ndani ya siku kumi (10) za kazi. |
| Tutatumia maoni yako kuborehsa huduma zetu. | • Tutaalika maoni na kutoa mawasiliano sahihi na ya kina katika taarifa za wateja wetu.<br>• Tutadumisha na kuripoti maoni yote kuzingatia ukaguzi na kuboresha huduma zetu. | Bila Malipo | Kuendelea |

Ikiwa kuna tashwishwi kuhusu huduma aliyopokelewa ofisini, tafadhali tuma malalamishi, maoni au mapendekezo kwa **Meneja wa hazina la eneo bunge, ofisi ya hazina ya maendeleo ya eneo bunge la Kabondo Kasipul, sanduku la posta 84-40223 Kadongo, Kenya ama barua pepe kwenye anwani: cdfkabondokasipul@ngcdf.go.ke / cdfkabondokasipul@gmail.com** au wasilisha malalamishi, maoni au mapendekezo kwenye sanduku la maoni na malalamishi yaliyo ofisini.